

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA KONDOA (KONDOA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-015-2018/2019

Mnamo tarehe 9 Novemba 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Kondoa (Kondoa WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani							
Daraja 1 (0- m ³ 10)	540	171%	1,464	2%	1,490	3%	1,542
Daraja 2 (11- m ³ 25)	625	171%	1,695	2%	1,725	3%	1,785
Daraja 3 (>m ³ 25)	665	171%	1,803	2%	1,835	3%	1,899
Taasisi	645	171%	1,749	2%	1,780	3%	1,842
Biashara	650	171%	1,763	2%	1,794	3%	1,856
Magati	1,000	150%	2,500	0%	2,500	0%	2,500
Viwanda	-	-	1,790	1%	1,810	2%	1,850

Jedwali Na 2: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi /Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	5,500	204%	16,695	3%	17,250	3%	17,785
Ofisi za Umma, Shule za Kutwa	25,000	200%	75,000	0%	75,000	0%	75,000

Shule za Bweni na Magereza	75,000	100%	150,000	0%	150,000	0%	150,000
Hospitali ya Wilaya	240,000	142%	580,000	0%	580,000	0%	580,000
Biashara	25,000	200%	75,000	0%	75,000	0%	75,000
Misikiti na Makanisa	15,000	100%	30,000	0%	30,000	0%	30,000

Jedwali Na 3: Tozo za Huduma za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi /Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Inayopendekezwa			
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	
Majumbani	1,000	1,000			
Taasisi	1,000				
Biashara	1,000				
Viwanda	-				

Jedwali Na.4: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	22,500	Asilimia Ishirini (20%) ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013		
Taasisi	22,500			
Biashara	22,500			
Viwanda	-			

Jedwali Na.5: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadi liko (%)	2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	10,500	0%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Taasisi	10,500	0%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Biashara	10,500	0%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Viwanda	-	-	10,500	0%	10,500	0%	10,500

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kondoa, sababu kuu ya kuomba marekebisho ya bei ni mapato finyu yatokanayo na bei za sasa yasiyokidhi gharama za uendeshaji na matengenezo. Kondoa WSSA wameeleza kuwa bei na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo na kuboresha huduma ya maji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 30 Januari 2019** katika **Ukumbi wa CCM Wilaya ya Kondoa** uliopo Kondoa Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Kondoa, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha

hapo juu **ifikapo tarehe 6 Februari 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KATI, GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KONDOA**.

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)

2 Januari 2019